BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Saba – Tarehe 19 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

244. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kumekuwa na mtindo wa baadhi ya watendaji wa Taasisi za Umma kudharau maamuzi yanayotolewa na Mahakama. Hatua hiyo inaleta hasara kwa Serikali kulipishwa pale Mahakama inapolazimika kukazia amri zake kwa taasisi hizo.

Je, hatua gani Serikali itachukua kwa watendaji wanaodharau amri za Mahakama na kusababisha Serikali kulipishwa fedha.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

183. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uanzishwaji wa kidato cha tano na sita katika Skuli za Serikali, hasa zinazoendelea kujengwa.

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kuanzisha kidato cha tano na sita katika skuli za Serikali.

(b) Je, ni skuli ngapi ambazo zinatoa kitado cha tano na sita kwa Wilaya za Unguja na Pemba.

235. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu imefanya mabadiliko ya Mtaala wa Elimu kuwakaririsha wanafunzi na kupasi mitihani na kwenda kwenye mtaala unaozingatia mwanafunzi kupata ujuzi (Competent Based Carriculam). Pamoja na hatua hiyo nzuri, kuna changamoto ya uwezo wa walimu watakaoendana na mabadiliko hayo kwa vile fani mbalimbali zimeanzishwa ambazo ni dhahiri hakuna walimu wa kutosha au walioandaliwa tayari, mfano fani ya kuongoza watalii.

(a) Je, kuna mkakati gani wa kuwapata walimu wenye fani ambazo hapo awali hazikuwepo katika mtaala.

(b) Je, walimu waliopo wamesaidiwa vipi kupatiwa mafunzo ya kina (intensive training), ili kukidhi mahitaji ya mtaala mpya.

(c) Je, kiasi gani cha bajeti kimetengwa ili kukidhi mahitaji ya mafunzo kwa walimu.

## Wizara ya Fedha na Mipango:

31. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilitoa tangazo kwa umma la kubadilisha usajili wa vyombo vyote vya moto kwenda kwenye usajili wa namba mpya, jambo lililoleta wasiwasi na usumbufu mkubwa kwa wananchi ambao ni watumiaji wa vyombo hivyo hapa Zanzibar.

(a) Je, ZRA imepata wapi mamlaka ya kisheria ya kufanya maamuzi haya.

(b) Je, ni kampuni ipi iliyopatiwa zabuni ya kuzalisha vibati vya namba mpya za vyombo vya moto Zanzibar na kwa mkataba wa kiasi gani.

(c) Je, tathmini ya idadi ya vyombo vilivyosajiliwa na idadi ya mapato yaliyokusanywa iko vipi hadi sasa, tokea kuanza

kwa zoezi hilo la kubadilisha usajili.

203. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali ya awamu ya nane imefanya juhudi kubwa za kufungua milango ya vivutio kwa wawekezaji mbalimbali, wakiwemo wazalendo. Pamoja na juhudi hizo nzuri, yapo malalamiko ya wawekezaji wazalendo katika sekta ya usafirishaji uwanja wa ndege na bandarini, kutozwa kodi zinazofanana kama vile ongezeko la asilimia mbili (2%) ya bei ya tiketi na shilingi 10,000 ya kodi ya uwanja. Kadhalika, upande wa bandarini, kila tiketi kuna ongezeko la shilingi 5000 wakati huo huo wawekezaji kutoka nje hawatozwi kodi hizo.

(a) Je, kwanini wawekezaji wazalendo wanatozwa kodi zinazofanana (duplicate) katika huduma moja.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya kodi za namna hiyo na kuziondoa ili kuwapunguzia mzigo wawekezaji wazalendo wakuwe zaidi.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

138. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Maeneo ya Fumba na Micheweni ni maeneo ambayo kwa siku nyingi Serikali imeyatenga kuwa ni maeneo huru ya kiuchumi (Free Economic Zones).

(a) Je, ni hatua gani iliyofikiwa kiuwekezaji hadi sasa kwa upande wa Maeneo Huru ya Uwekezaji Micheweni.

(b) Je, ni wawekezaji wangapi wameshaonesha nia ya kuwekeza katika maeneo ya Micheweni hadi sasa.

(c) Je, ni hatua gani imefikiwa ya kuanza kwa miradi ya uwekezaji katika maeneo hayo ya Micheweni.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

24. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    Serikali imechukua hatua gani madhubuti katika kutatua migogoro ya ardhi inayowakumba wanawake ambao wengi wao hunyanyasika katika masuala ya urithi, umiliki na matumizi ya ardhi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

73. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

    Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuja na kasi kubwa ya utafutaji wa rasilimali ya mafuta na gesi hapa Zanzibar.

    Je, ni hatua gani imefikiwa katika utafutaji wa rasilimali hii muhimu sana kwa taifa.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

155. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

     Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mitaji, ili kuwawezesha kuongeza vipato vyao kupitia shughuli za ujasiriamali.

     (a) Je, Serikali imefanya tathmini ya kubaini ni kwa kiasi gani wananchi hawa wamenyanyuka kiuchumi kupitia fursa hii ya uwezeshaji wa Serikali.

     (b) Ni eneo gani la miradi ya ujasiriamali ambayo imetoa tija zaidi na miradi ipi ambayo haikufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

37. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

    Kwa muda mrefu sasa, barabara ya Kinoe Migombani ‘Store’

inayoelekea Jiso mpaka kutokezea Konde Msikiti wa Ijumaa Majenzi, ni mbovu na haipitiki hasa zinaponyesha mvua. Hali inayoendelea kuwaletea usumbufu mkubwa wananchi wanaoitumia barabara hiyo katika shughuli zao za kila siku.

Ni lini Serikali itaijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

119. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barabara inayokwenda Skuli ya Dkt. Ahmed Salim hutumiwa na watu wa maeneo mbalimbali. Kwa kuwa barabara hii ni mbovu na inaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa vyombo na wanaotembea kwa miguu.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

20. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ina mikakati ipi ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hasa katika maeneo ya vijijini, ili kuongeza uzalishaji wa kilimo na kupunguza utegemezi wa chakula kutoka nje ya Zanzibar.

246. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mradi wa kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji umefanyika kwa awamu mbili na zote zimekamilika na wakulima waliopo mwanzo walitakiwa kurejeshwa kwenye mashamba yao.

(a) Je, wakulima wangapi waliokuwa wanalima mwanzo kwenye bonde la Cheju wamerejeshwa na wangapi waliokuwa hawakurejeshwa, na kwa sababu gani hawakurejeshwa.

(b) Je, utaratibu gani umetumika katika kugawa mashamba (plots) kwa wakulima katika bonde la Cheju.

**Wizara ya Afya:**

61. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tatizo la afya ya akili limekuwa kubwa sasa katika maeneo mbali mbali.

Ni upi mpango wa Serikali wa kupambana na matukio yanayojitokeza ya tatizo la afya ya akili hasa kwa watoto wetu.

136. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Abdalla Mzee ni moja ya hospitali tegemeo kwa wananchi wote wanaoishi Pemba ambao rufaa katika Hospitali za Wilaya hupelekwa hapo kwa matibabu zaidi. Ni miezi kadhaa sasa kumejitokeza changamoto ya kukosekana kwa vipimo vyote muhimu kwa wagonjwa wanaofikishwa katika hospitali hiyo.

(a) Kwa kuwa Serikali inaitambua changamoto hii, ni hatua gani imezichukua kuiondoa ili kuokoa maisha ya wananchi wanaofikishwa katika Hospitali ya Abdalla Mzee.

(b) Ni yepi makubaliano ya uendeshaji wa hospitali hii baina ya Serikali na Wachina ambao walikuwa wakiiendesha hospitali hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

227. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Zamani, Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, namba 7/2013 (ZURA) iliruhusu wananchi kutoa maoni yao kabla ya kupandishwa kwa bei ya umeme lakini hivi sasa utaratibu huo umeondolewa baada ya Baraza la Watumiani Nishati kufutwa kwenye sheria hiyo na bei za umeme sasa kupandishwa bila ya kuulizwa watumiaji.

(a) Baada ya kuondoshwa Baraza la Watumiaji Nishati, je, hivi sasa utaratibu wa kuwashirikisha wananchi kabla ya kupandishwa kwa bei ya umeme unafanyika vipi.

(b) Kuna sababu gani za msingi za kufuta Baraza la Watumiaji Nishati.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

221. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wananchi wanaofanya shughuli zao ndani ya Mamlaka ya Mji Mkongwe kukamatwa na wakati mwengine kupigwa na askari wa Mamlaka ya Mji Mkongwe.

(a) Je, ni sheria gani zinawapa uwezo askari wa Mji Mkongwe kukamata na wakati mwengine kupiga watu na kuwashikilia.

(b) Je, askari hao wa Mamlaka wanao ujuzi na taaluma ya kukamata na kuweka kizuizini watu wanaowakamata kwa taratibu zinazotambulika na sheria za nchi.

## II. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**

**Zanzibar,**
**19 Februari, 2026.**